www.xtrapapers.com

M12/1/A1SWA/SP1/SWA/TZ0/XX

22120299

International Baccalaureate®
Baccalauréat International
Bachillerato Internacional

**SWAHILI A1 – STANDARD LEVEL – PAPER 1**
**SWAHILI A1 – NIVEAU MOYEN – ÉPREUVE 1**
**SWAHILI A1 – NIVEL MEDIO – PRUEBA 1**

Thursday 10 May 2012 (morning)
Jeudi 10 mai 2012 (matin)
Jueves 10 de mayo de 2012 (mañana)

1 hour 30 minutes / 1 heure 30 minutes / 1 hora 30 minutos

---

INSTRUCTIONS TO CANDIDATES

- Do not open this examination paper until instructed to do so.
- Write a commentary on one passage only. It is not compulsory for you to respond directly to the guiding questions provided. However, you may use them if you wish.
- The maximum mark for this examination paper is *[25 marks]*.

INSTRUCTIONS DESTINÉES AUX CANDIDATS

- N'ouvrez pas cette épreuve avant d'y être autorisé(e).
- Rédigez un commentaire sur un seul des passages. Le commentaire ne doit pas nécessairement répondre aux questions d'orientation fournies. Vous pouvez toutefois les utiliser si vous le désirez.
- Le nombre maximum de points pour cette épreuve d'examen est *[25 points]*.

INSTRUCCIONES PARA LOS ALUMNOS

- No abra esta prueba hasta que se lo autoricen.
- Escriba un comentario sobre un solo fragmento. No es obligatorio responder directamente a las preguntas que se ofrecen a modo de guía. Sin embargo, puede usarlas si lo desea.
- La puntuación máxima para esta prueba de examen es *[25 puntos]*.


© International Baccalaureate Organization 2012

www.xtrapapers.com



*Toa maoni yako juu ya* ***moja*** *ya tungo zifwatazo.*

**1.**

“Ati barua kutoka kwa Janeti?! Ni kusema kwamba aliende wapi?! Anaweza kuwa aliamua kurudi adabu kweli?!” Korneli alikuwa na wasiwasi kidogo wakati akiuliza maswali hayo.

“Barua yenyewe ndiyo hii. Isome kwa makini nawe utafahamu kule alikoenda Janeti,” Harry alimkabidhi barua hiyo, na kimya kirefu kikatawala kati yao wakati Korneli akisoma.

Mpenzi wangu Korneli,

Ni mwingi wa haraka na wasiwasi ninapokuandikia barua hii kama mawasiliano ya mwisho kati yangu nawe. Tulijuana bado tukiwa wadogo huko kwetu Adabu natumekuwa kama watoto mapacha hadi sasa, siku hii ambayo ukatili wa dunia umetutenganisha daima. Nakutakia maisha mema na ya ufanisi huko kifungoni ulikotupwa. Mapenzi niliyonayo kwako hadi wakati huu mgumu ninapokuandikia barua hii, yangali ni mengi kama mchanga wa bahari; hayajapungua kwa tone lolote licha ya mambo makubwa yaliyotokea. Siwezi kuyakabili maisha bila kuwepo nami. Figa limoja la meko linapovunjika, mawili yaliyosalia hukosa Umuhimu wake kwa kazi ya upishi. Kwa vile dunia imenionea na imenikataa, hata mimi nimeikataa. Sina shaka kwamba ni mapenzi yako mengi uliyonayo kwangu, na roho yako safi ya kutushughulikia mimi na mwanao, ndio mambo yaliyokuongoza katika jaribio la unyanganyi hadi ukafungwa jela. Kwa sasa, ninaamini, kuzidi upeo wa imani yangu kwamba dunia, mimi na wewe katu hatutaonana tena ila akhera. Maisha yangu yote yamekuwa na aibu na majuto tangu penzi letu lilipochipuka miaka minne iliyopita tukiwa wanafunzi wa kidato cha kwanza. Kwa sasa, ulivyotoweka maishani mwangu, sina tumaini lolote na sitaki kuanza upya katika maisha. Sitapenda kupenda zaidi ya jinsi nilivyokupenda. Ninapomtazama mtoto wetu, machozi hayeshi mwangu ninapomuona anavyokupenda na kukuhitaji wewe kama babake. Kwangu, mimi na yeye ulimwengu si mahali pazuri pa kuishi. Hukuwa na kazi wala pesa lakini tulikuonea fahari kama mmoja wetu; kichwa cha nyumba yetu. Tulifurahia juhudi zako kutapatapa kule nje ukitutafutia maisha kama familia yako, huku matumaini yakiwa mengi kwamba siku moja utafaulu ili nasi pia tufurahie maisha. Lakini kwa bahati mbaya, umepoteza yote. Kupoteza kwako kumeipoteza radha ya maisha katika roho yangu na ile ya mwanetu. Kwa sababu hiyo, tumeamua ni vizuri kuyatamatisha maisha yetu kwa sumu ya kuulia panya kama njia ya pekee ya kutupa pumziko la milele. Endapo utatoka kifungoni mzima na salama, ombi langu ni moja: Yapange maisha yako upya na ufanikiwe. Tukumbuke mimi na mwanao mnamo kila siku ya uhai wako. Kwa wakati huu langu ni kumuomba Rabuka msamaha wa dhati kutokana na maovu yote ya uhai wangu, na hasa dhambi hii ya sasa ya kuyakatiza maisha ya kiumbe kisicho na hatia; mwanetu, na maisha yangu mwenyewe. Ninakuomba nawe msamaha kwa kitendo hiki kiovu. Kwa heri ya milele tuonane tena kwake kwema. Mola awe nawe daima. Picha zangu na za mwanetu ndizo hizo. Zihifadhi ukitukumbuka kila siku.

Nimesalia wako kwa uaminifu hadi mwisho wa kosa;

JANETI

www.xtrapapers.com



Baada ya kuisoma barua hiyo, huzuni wa bayana ulimzidi Korneli, akadondokwa machozi bila yeye kupenda. Aliomboleza moyoni mwake na kumuomba Mungu mhisani kuziweka roho za Janeti na mwanawe pahali pema peponi.

"Mungu! Msamehe Janeti dhambi ovu ya kuyaondoa maisha, na uziweke roho zao wawili peme peponi hadi tuonane tene siku ya hukumu juu mbinguni- AMINA."

"Sasa wanuia kufanya nini katika maisha yako Kornel?" Harry alimuuliza alipokamilisha kuisoma barua hiyo.

"…lazima sasa niafikiane na mafundisho ya mababu wetu kuwa mwenda tezi na omo marejeo ni ngamani." …Nitaondoka niende kwa baba yangu na kumuambia "baba, nilikosa juu ya mbingu na mbele yako. Sistahili kuitwa tena mwanao. Ukipenda, nichukue na unipe hadhi ya mtumishi wa kwako nyumbani. Ni tayari hata bila mshahara."

Moses Amoke Andere, *Uhondo mchungu* (2005)

– Mwandishi anatumia mbinu gani katika kupitisha ujumbe wake?

– Onyesha vile mwadishi anavyofaulu kuyateka mawazo ya wasomi wake kwanzia mwanzo hadi mwisho.

– Hisia zinazoimbuka kwenye kifungu hiki zinaonyesha nini kuhusu maisha kwa ujumla.

– Kulingana na matukio haya, onyesha uhusiano uliopo katika hali halisi.

www.xtrapapers.com



**2.**

**Kila mchimba kisima**

Tenda utendapo tendo, tenda tendo kwa hekima,
Liandamane mwenendo, sawa na yako kalima,
Kalima yenye upendo, kufurahisha mtima,
Kila mchimba kisima, budi huingia mwenyewe.

Utendapo la faraja, tendo ni yako salama,
Yakukupa kila tija, na ushindi wa daima,
Upate njema faraja, duniani na kiyama,
Kila mchimba kisima, budi huingia mwenyewe.

Utendapo la miuja, tendo ni yako na kama
Ya kukutia harija, hasara kukuandama,
Usione ufuwaja, mwanzo na yako hatima,
Kila mchimba kisima, budi huingia mwenyewe.

Nakwambia uelewe, pulika ninayosema,
Si ari ya mwenginewe, kumuonya kwa lazima,
Mtu hufunza mwanawe, kwanza ajue heshima,
Kila mchimba kisima, budi huingi mwenyewe.

Nisipokwambua wewe, kukufunza kila njema,
Kusudi nikuongoe, uepuke na tuhuma,
Matusi ndimi nipawe, ila na kila lawama,
Kila mchimba kisima, budi huingia mwenyewe.

Hii si kheri ujue, matusi kunigandama,
Hadhi usiniuzuwe, hamithilishwa na nyama,
Fikiri moyo utuwe, nikupapo taaluma,
Kila mchimba kisima, budi huingia mwenyewe

Shika tena utambuwe, wasio huu ni mwema,
Matendo usipunguwe, mazuri kutenda hima,
Yatende ubarikiwe, upawe na taadhima,
Kila mchimba kisima, budi huingia mwenyewe.

Yakupasa uchunguwe, kila jambo kulipima,
Upime ufafanue, mambo yote kwa alama,
Lakuwaka ulijue, pia lipi la kuzima,
Kila mcimba kisima, budi huingia mwenyewe.

Muriithi Gituma, *Kurunzi ya Ushairi* (2010)

www.xtrapapers.com



- Onyesha vile muundo na mtindo unaotumiwa na mwandishi unavyosaidia kupitisha ujumbe.
- Onyesha jinsi lugha anayoitumia mwandishi inavyofanikisha katika kupitisha ujumbe.
- Onyesha jinsi mwandishi anavyotumia mbinu mbalimbali za utunzi wa mashairi.
- Mtunzi amelenga hadhira gani katika shairi hili na kwa nini?